

UTANGULIZI

USCF CCT TAKWIMU ni umoja wa wanafunzi wa Kikristo wa Chuo cha Takwimu chini ya CCT na Chaplaincy ya UDSM. Kwa kutii agizo la Yesu Kristo, tulifanya huduma ya uinjiliisti katika Halmashauri ya Nanyamba, Mtwara, mwezi Februari 2025, tukiwa na lengo la kuwahudumia kiroho na kijamii.



HUDUMA YA UINJILISTI WA NYUMBA KWA NYUMBA

Tulifanya uinjiliisti kwa siku nne, tukihubiri Injili na kusambaza vipeperushi nya mafundisho ya Neno la Mungu. Jumla ya watu 194 walifikiwa, na 97 walimpokea Kristo.



SHUKRANI NA HITIMISHO

Tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kufanikisha huduma hii na kwa wote walioituunga mkono kwa hali na mali. Tunathamini msaada wa waumini, wachungaji, na makanisa yote yaliyotushika mkono katika maombi na sapoti. Mungu aendelee kubariki huduma hii! AMEN.



USCF CCT TAKWIMU

Follow us on



USCF_CCT TAKWIMU

USCF CCT TAKWIMU
WE SERVE THE LIVING GOD

NANYAMBA MISSION OUTREACH

*"Enendeni ulmwenguni mwote,
mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."*
(Marko 16:15)



MKUTANO WA INJILI NA SEMINA YA NENO LA MUNGU (CRUSADE)

Kwa siku saba, mikutano ilifanyika kila jioni, ikiambatana na mahubiri, nyimbo, na maombi. Watu 117 walimpokea Kristo, wagonjwa 47 waliombewa, na 31 walipokea uponyaji.

HUDUMA YA KUTOA ELIMU MASHULENI

Tuliwahamasisha wanafunzi juu ya maadili na elimu, huku washirika wetu wakifundisha masomo kwa wanafunzi kutokana na upungufu wa walimu. Jumla ya wanafunzi 1,534 walihudumiwa.



SIKU MAALUMU YA MFUNGO NA MAOMBI

Ijumaa ilitengwa kwa maombi maalum kwa Nanyamba, Mtwara, taifa, na wote waliouunga mkono huduma hii.



HUDUMA YA MATENDO YA HURUMA



- Hospitali: Tulifariji na kuwaombea wagonjwa 19 katika Kituo cha Afya Mt. Hildegard Nanyamba.
- Shule: Tulitoa vifaa kwa wanafunzi wenyewe uhitaji, wakinufaika wanafunzi 1,534.



UINJILISTI KWA NJIA YA SINEMA

Filamu za Kikristo zilioneshwa kila jioni, zikihamasisha watu kuelewa na kuimarisha imani yao.

HUDUMA ZA JAMII NA KAZI ZA MIKONO

Washiriki walijuhisha na usafi, mapishi, na kazi za mikono, wakionesha mshikamano wa Kikristo.

